ISO 9001:2015 Certified

# The Regulator

JARIDA LA KILA ROBO MWAKA LA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

Linatolewa bure

ISSN: 0856 - 8030 | NA. 1/2024 | JANUARI - MACHI 2024



## Tanzania yazidi Kupaa

- Yapata nafasi kurusha setilaiti yake
- Taifa lajiandaa utangazaji wa redio kidijitali

# TUNU KUU




## Weledi

Tunatekeleza majukumu yetu kwa kutoa huduma bora tukizingatia maadili na heshima kwa wateja wetu.

## Ubunifu

Tunazingatia ubunifu katika kushughulikia masuala ya kiudhibiti sanjari na mabadiliko ya teknolojia duniani.

## Uadilifu

Tunatekeleza kazi zetu kwa kuzingatia maadili, uthabiti na uaminifu wa hali ya juu.

## Utendaji wa Pamoja

Tunaamini katika utendaji kazi wa pamoja ili kutatua matatizo na kutambua kwamba mawasiliano imara ni muhimu katika kujenga mazingira ya ushirikiano.

## Uwajibikaji

Tunawajibika kikamilifu na kuchukua dhamana tunapotoa huduma.

ISSN: 0856 - 8030
NAMBA YA USAJILI: 00000115
Na. 1/2024. JANUARI - MACHI, 2024

# The Regulator

Hili ni toleo la Kiswahili la jarida la The Regulator, linalotolewa mara nne kwa mwaka na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA). TCRA ni taasisi ya serikali inayosimamia mawasiliano ya kielektroniki na posta nchini. Jarida hili ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

## TCRA ina wajibu katika majukumu yafuatayo:-

1. Kuhimiza ushindani bora na uchumi wenye tija;
2. Kulinda haki na maslahi ya watumiaji;
3. Kuhamasisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wote (wakiwemo Walemavu) ukijumuisha watumiaji wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji ambao wako katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara;
4. Kuimarisha elimu kwa umma, uelewa na kuzifahamu huduma zinazosimamiwa;
5. Kuhakikisha umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

## BODI YA WAHARIRI

**Mwenyekiti**
Mhandisi. Mwesigwa Felician

**Katibu**
Bw. Rolf Kibaja

**Wajumbe**
Bw. Semu Mwakyanjala (Mratibu)
Dkt. Philip Filikunjombe
Dkt. Peter Kihogo
Bw. Peter Lyimo
Bw. Robin Ulikaye
Bw. Abel John
Bi. Vitalia Kidabulo
Bw. Alpha Wawa

**Mhariri Uzalishaji**
Bw. Isaac Mruma

**Anwani ya ofisi za uhariri**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu: +255 784558270, +255 784558271.
Barua pepe: regulator.magazine@tcra.go.tz; dg@tcra.go.tz
@tcra_tanzania

**Ofisi Kuu**
Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 474,
Postikodi 14414 Dar es Salaam.
Simu +255 784 558270-1 Simu ya bure: 0800008272.
Barua pepe: dg@tcra.go.tz. Tovuti: www.tcra.go.tz

**Ofisi ya Zanzibar**
Na. 19 Mbuyukisutu, Mjini Magharibi, Zanzibar.
S.L.P 3284,
Postikodi 71194 Mjini Magharibi
Simu: +255 24 2235062
Baruapepe: zanzibar@tcra.go.tz

**Kanda ya Kaskazini**
Jengo la PAPU, Ghorofa ya kumi na mbili. 280 Barabara ya Moshi-Arusha. S.L.P 15675,
Postikodi 23194 Arusha.
Simu: +255 272970286
Baruapepe: arusha@tcra.go.tz

**Kanda ya Kati**
LAPF Plaza, Ghorofa ya nne. Na. 2 Mtaa wa LAPF.
S.L.P 2229,
Postikodi 41194 Dodoma. Simu: +255 262321731
Baruapepe: dodoma@tcra.go.tz

**Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
Jengo la NHIF, Ghorofa ya tano. Na. 7 Barabara ya Karume.
S.L.P 1375,
Postikodi 53194 Mbeya. Simu: +255 25 250 5016
Baruapepe: mbeya@tcra.go.tz

**Kanda ya Ziwa**
Jengo la NSSF Mafao, Ghorofa ya nne, upande B Na.13 Jomo Kenyatta Avenue.
S.L.P 3108,
Postikodi 32194 Mwanza. Simu: +255 28 2505082,
Baruapepe: mwanza@tcra.go.tz

**Kanda ya Mashariki**
Na.147 Barabara ya Kajenge, Mikocheni,
S.L.P 35615,
Postikodi 14194 Dar es salaam.
Simu: +255 22 2775110
Baruapepe: easternzone@tcra.go.tz

# Yaliyomo

04 Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



14 Wito Bodi ya Ithibati iharakishwe




06 Tanzania yavuna Mkutano wa Masafa Duniani





Makala kuu

16 Kanuni kuongeza ufanisi matumizi postikodi





Mapya kwenye sheria

08 Tanzania yajiandaa kwa Utangazaji wa redio Kidijitali



17 Takwimu sekta ya Mawasiliano



BARUA YA MHARIRI

# Huduma za utangazaji kwa wote

Utangazaji ni mojawapo ya maeneo muhimu yanayosimamiwa na Mamlaka ua Mawasiliano Tanzania (TCRA). Usimamizi pia uko kwenye mawasiliano ya simu, intaneti na huduma za posta na usafirishaji vifurushi.

Kuwepo kwa makala nyingi kuhusu utangazaji kwenye toleo hili kunalenga kuinua uelewa wa wasomaji na wadu wengine kuhusu masuala ya utangazaji na maudhui.

Msisitizo uko kwenye mambo mapya matatu yanayohusu miundombinu ya kuhakikisha matangazo yanafikia wasikilizaji na watazamaji wengi zaidi, na pia kuboresha ubora huduma za maudhui.

Mambo hayo ni pamoja na Tanzania kupata nafasi anga za juu kwa ajili ya setilaiti yake ya kwanza ya mawasiliano, na mpango wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kujenga miundombinu ya utangazaji ili kufikisha matangazo maeneo yenye ugumu kufika mawimbi ya redio na televisheni.

Aidha TCRA imeainisha maeneo yenye huduma hafifu na yasiyo na huduma za mawasiliano ya simu na intaneti baada ya kufanya utafiti nchini kote. Imewasilisha taarifa ya utafiti huo kwa huduma ili waboreshe huduma kwenye maeneo hayo.

Madhumuni ni kuwezesha huduma za mawasiliano kufikishwa maeneo yanayoonekana hayana 'mvuto' kibiashara, kwa wawekezaji na ambayo hayajafikiwa na huduma ipasavyo.

Haya yote yamekuja sawia na mpango wa Tanzania kuanzisha huduma za utangazaji wa redio kidijitali ili kuwezesha vituo zaidi vya redio kuanzishwa sambamba na vile vilivyopo vinavyotumia masafa kwenye bendi za AM au FM.

Utangazaji wa redio kidijitali, unaojulikana kama DSB, kifupisho cha *Digital Sound Broadcasting*, unatumia masafa na nishati kwa ufanisi zaidi na vifaa vyake ni rahisi kwa wasikilizaji kutumia.

Pamoja na hayo, TCRA inatekeleza mpango wa kushirikisha wadau kuendeleza ubora wa maudhui ya utangazaji kwa lengo la kulinda tunu za taifa Tanzania na kuhakikisha maudhui yanazalishwa na kusambazwa kwa kuzingatia kanuni, miongozo na miiko iliyowekwa.

TCRA inasimamia utangazaji Tanzania Bara, na inayo kamati mahsusi inayoshughulikia maudhui. Kamati hiyo inafuatilia uzingatiaji maadili na kanuni za maudhui ya redio, televisheni na mtandaoni kwa wenye leseni ya Mamlaka.

Mamlaka ina mipango ya elimu inayolenga kujenga uelewa wa kanuni za utangazaji miongoni mwa wadau. Tangu mwaka 2007 TCRA inafanya mikutano ya mwaka ya utangazaji.

Washiriki wa mkutano wa mwaka 2024 wametaka hatua zichukuliwe haraka kuanzisha Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari.

Bodi hiyo inatarajiwa kuwa na mchango mkubwa katika kuhakikisha sekta ya utangazaji inazingatia maadili, kanuni na weledi katika utendaji kazi wake. Bodi ya TCRA imeundwa chini ya Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016.



*Watangazaji ndani ya studio za Korogwe fm redio*

# Uendelezaji juhudi za pamoja, uvumbuzi



Dkt. Jabiri K. Bakari, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA

Wapendwa Wasomaji,
Ninayo furaha kubwa kuwaletea toleo hili la jarida letu, ambalo linawasilisha masuala yaliyojitokeza kwenye safari yetu hadi robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2023/2024.

Sekta kwa Robo ya Tatu ya Mwaka wa Fedha 2023/24 (Januari hadi Aprili 2024). Tunaanza Makala kuu kwa kushajihisha ina umuhimu wa kipekee. Inaelezea mafanikio makubwa yaliyopatikana katika Mkutano wa Kimataifa wa Mawasiliano ya Redio, (WRC-23) uliofanyika Dubai, Falme za Kiarabu, kuanzia tarehe 20 Novemba 2023 hadi 15 Desemba 2023. Kwenye mkutano huo, unaojulikana kama WRC-23, ambapo nchi yetu ilipata manufaa kadha wa kadha. kama inavyoainishwa kwenye Makala kiongozi ya jarida hili iliyotambulishwa kwenye ukurasa wa mbele.

Matokeo ya jitihada zilizofanywa kwenye Mkutano huu ni pamoja na Tanzania kupata upatikanaji wa masafa zaidi ya mawasiliano ya simu, kuwezesha mawasiliano ya kasi kubwa. Masafa haya yanatumika kwa huduma nyingi, zikiwemo , usafiri wa majini na usalama wake, uongo-zaji wa ndege na usalama wa anga na, utabiri wa hali ya hewa.

Matumizi mengine ni kwa mawasiliano katika kutabiri na kugundua majanga, utangazaji wa televisheni, mawasiliano ya simu na intaneti. Aidha mafanikio mengine ni upatikanaji masafa kwa ajili ya matumizi ya rada na ukusanyaji wa taarifa kupitia obiti za satelaiti.

Upangaji wa masafa ulizingatia kanuni muhimu ya kila nchi kupata haki sawa katika upatikanaji wa masafa na obiti za satelaiti, kulingana na ibara ya 44 ya Katiba ya Umoja wa Shirika la wa Mawasiliano Duniani (ITU).

Matokeo ya mkutano wa WRC-23 yanaimarisha misingi ya kukuza sekta ya mawasiliano Tanzania, na hivyo kuboresha kiwango cha maisha ya kila mwananchi.

Mafanikio haya yanatokana na jitihada za pamoja na kutekeleza wajibu kikamilifu kunakofanywa na wataalamu wetu kila mara wanapoiwakilisha nchi kwenye mikutano ya kimataifa inayojadili masuala ya Kisekta.

> Matokeo ya WRC-23 yanatoa mwanga wa mafanikio ambayo, tukiungana kama wadau wa sekta, yataleta ukuaji mkubwa wa sekta ya mawasiliano.

Napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza timu ya Wataalamu wa TCRA pamoja na wawakilishi wetu wengine kwenye Mkutano huu kwa kazi nzuri ya kutetea nafasi ya nchi yetu.

Kujitolea kwao kwa dhati kumewezesha uwekaji wa misingi ya mabadiliko chanya ambayo yatapatikana kwenye sekta sasa na baadae.

Mbali na ujumbe kuhusu mafanikio ya nchi yetu wakati wa Mkutano wa WRC 23 pia toleo hili linabeba maudh-ui kuhusu kikoa cha DOT TZ ambacho ni utambulisho halisi wa Tanzania kwenye mtandao, pia imo Makala ya rejea za kanuni za sekta ambazo sasa zinatafsiriwa katika Kiswahili, dondoo za Usalama kwenye mtandao, takwimu za sekta kwa robo ya pili ya mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makala mbalimbali za uelewa wa sekta ya mawasiliano.


Ninawasihi wote tuungane kuendeleza juhudi za pamoja zinazoweza kuleta mabadiliko makubwa. Kwa pamoja, tunaweza kuendeleza sekta na kuiwezesha Tanzania kuunganishwa zaidi kimawasiliano.

Ninapohitimisha ujumbe huu ningependa kuwaasa wadau wote kuendelea kushiriki kikamilifu katika kuwahamasisha vijana wetu kutumia kikamilifu fursa zinazojitokeza katika ulimwengu wa kidjitali.

Hii ni pamoja na wao kujifunza masuala yanayohusu teknolojia za kidijiti kupitia klabu za Kidijiti zinazoanzi-kshwa katika shule na vyuo. Klabu hizi zinatoa hamasa kwa vijana kujifunza masomo ya Hisabati, Sayansi, Teknolojia, na Uhandisi ambayo yatawaweze-sha vijana kuwa washiriki kamili wa kujenga uchumi wa kidijitali.

Kwa kufanya hivyo tutakuwa tunakiandaa kizazi kipya kiweze kufanyia kazi maazimio ya mkutano wa WRC-23 na hivyohivyo kwa masuala mengine yanayojitokeza kwenye sekta hii yenye mabadiliko mengi.

Nawatakieni kila la heri!



**TAARIFA**

# Bodi ya TCRA yakamilika

Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imekamilika baada ya wajumbe wapya wanne kuteuliwa 21 Machi mwaka huu.

Wataungana na Mwenyekiti, Dkt Jones A. Killimbe na Makamu Mwenyekiti, Bw. Juma Hassan Reli ambao waliteuliwa na Rais Mh. Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania mapema; na Mkurugenzi Mkuu, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari.

Walioteuliwa ni Profesa Aloys Ntaturo Mvuma, Dkt. Hanifa Twaha Masawe, Dkt. Irene Charles Isaka na Bw. Mohamed Ame Makame.

Wajumbe hao wanne wameteuliwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye kwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ya 2003.

Bodi ya Wakurugenzi ya TCRA ni chombo cha juu cha uongozi wa Mamlaka na ina wajumbe saba. Kuna Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti (wasio-watendaji na ambao wanateuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania), wajumbe wanne wasio watendaji (ambao wanateuliwa na Waziri anayesimamia sekta ya mawasiliano).



**Dr. Jones A. Killimbe**



**Mr. Juma Hassan Reli**



**Prof. Aloys Ntaturo Mvuma**



**Dr. Hanifa Twaha Masawe**



**Dr. Irene Charles Isaka**



**Mr. Mohamed Ame Makame**



**Dr. Jabiri K. Bakari**

# Tanzania ‘yavuna’ Mkutano wa Masafa Duniani

Na Rolf Kibaja, aliyekuwa Dubai, hivi karibuni

## Yapata nafasi angani kurusha setilaiti yake

Tanzania ilishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Upangaji wa Masafa ya Mawasiliano na Obiti za Satelaiti, unaojulikana kwa kifupi kama WRC-23 jijini Dubai, Falme za Kiarabu, Desemba 2023, ambako nchi ilifanikiwa katika maeneo mengi.

Tanzania ilipata nafasi angani (obiti) ya kurushia setilaiti yake na imeongezewa masafa kwa huduma za aina mbalimbali. Masafa hayo ni pamoja na yatakayowezesha huduma ya intaneti ya kasi kwa kutumia uzao wa tano wa simu za mkononi (5G).

Masafa mengine ni ya mawasiliano kwenye usafiri wa majini, uongozaji ndege, huduma za satelaiti kwa matumizi ya hali ya hewa, utabiri na ugunduzi wa majanga na vihatarishi, utangazaji wa televisheni, na matumizi ya rada.

Kupatikana obiti ni fursa kwa Tanzania kujikita katika tafiti na kurusha setilaiti ambayo itawezesha maendeleo ya utangazaji. Fursa nyingine ni kwa wawekezaji kuangalia namna ya kuwa na Satelaiti ambayo itasaidia wananchi kupata mawasiliano ya utangazaji kupitia vituo vya redio na televisheni.

Vituo vingi vya utangazaji Tanzania na nchi nyingi za Afrika vinatumia setilaiti za mataifa mengine; hivyo kufanya gharama za uendeshaji kuwa kubwa.

Obiti ya Tanzania ipo nyuzi 16 magharibi katika obiti ambayo inakuwa juu ya maeneo kijiografia wakati wote dunia inapozunguka jua, yaani geostationary.


Masafa ya kasi Tanzania iliyopewa yako katika wigo wa masafa wa megahezi (MHz) 3600 hadi 3800. Haya yanafanikisha huduma za mtandao wa kasi kwa mawasiliano ya simu na vifaa vya mkononi.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye aliyeongoza ujumbe wa Tanzania, amesema upatikanaji wa masafa haya utaendelea kuchochea maendeleo makubwa ya uchumi wa kidijiti ambao unahitaji intaneti ya kasi.



Utawezesha Watanzania wengi zaidi kupata huduma mbali mbali katika jamii kama vile huduma za benki, fedha, usafirishaji, kilimo, utalii, miundombinu, elimu na afya kupitia mitandao, aliongeza.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari alisema ugawaji wa megahezi 3600-3800 utawezesha matumizi ya teknolojia ya uzao wa tano (5)G nchini, na kuongeza kasi ya intaneti.




Aidha masafa hayo yatapanua wigo wa mtandao wa simu, na kuchochea ukuaji wa kiuchumi kupitia ubunifu na uzalishaji wenye tija kwa kutumia teknolojia za mawasiliano ya kidijiti,' alisisitiza Dkt Bakari.

Mkutano wa WRC-23 ulitoa nafasi ya kuwa na vifaa vya mawasiliano ambayo vitawekwa juu angani kutoka kilometa 20 hadi 50 kutoka usawa wa bahari, na kuweza kufanya kazi kama inayofanywa na minara ya ardhini ya mawasiliano.

Dkt Bakari alifafanua kuwa hii itawezesha upatikanaji wa mawasiliano bora ya simu na intaneti na kuongeza ufanisi sehemu zisizopata huduma ya mawasiliano kama vile vijijini.

Alieleza kuwa mkutano huo vilevile ulijadili matumizi ya televisheni za Kidijitali kwenye bendi ya UHF. Majadiliano pia yalihusu uwezekano wa kutumia sehemu ya masafa ya bendi hiyo kwa huduma za simu na intaneti baadae bila kuathiri huduma za utangazaji kwenye bendi hii ndani ya nchi na nchi jirani.

Dkt Bakari amesema kupatikana kwa masafa na nafasi kwenye obiti ya setilaiti kunafungua njia kwa mawasiliano bora na teknolojia ya kisasa.

Ameongeza kuwa TCRA imejiandaa kusimamia eneo hili jipya la miundombinu ya setilaiti.

Mikutano ya WRC inaandaliwa na Shirika la Kimataifa la Mawasiliano Duniani (ITU) kila miaka mitatu (3) hadi minne (4). Ajenda zake ni kupitia, na ikibidi kurekebisha kanuni za mawasiliano, ambazo ni mkataba wa kimataifa unaosimamia matumizi ya masafa na obiti za satelaiti, kwa kuzingatia mabadiliko ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Akizungumza na ujumbe wa Tanzania katika kikao-kazi baada ya mkutano huo, Mhe. Nnauye aliwataka wataalamu kuanza kujipanga kuchukua hatua za utekelezaji wa makubaliano ya mkutano.

Wanapojipanga washirikishe wadau mbalimbali juu ya mwelekeo wa sekta ya mawasiliano, na kuchangamkia fursa zinazotokana na mabadiliko ya TEHAMA duniani, aliongeza.



UTANGAZAJI

# Tanzania yajiandaa kwa utangazaji wa redio kidijitali

Na Lokila Mosso

Miaka 10 baada ya kuhama kwa mafanikio makubwa kutoka utangazaji wa televisheni wa analojia kwa mifumo ya ardhini kwenda dijitali, Tanzania inakamilisha mipango kuanza matumizi ya teknolojia bora zaidi ya utangazaji wa redio kidijitali.

Teknolojia hiyo, ambayo inatumia masafa ya utangazaji wa ufanisi zaidi, itaenda sambamba na iliyopo ya FM inayotolewa na vituo 234 vya redio Tanzania Bara.

**234** **Stesheni za redio za FM Tanzania Bara**

Hakuna tarehe ya kuhama kama ilivyokuwa kwa utangazaji wa televisheni kidijitali.

Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU), ambayo ni taasisi ya umoja wa mataifa inayosimamia teknolojia ya habari na mawasilino (TEHAMA) inasisitiza kwamba tofauti na kipindi cha kuhamia utangazaji televisheni kidijitali, hakuna tarehe ya mwisho ya utangazaji wa redio kwa analojia.

Teknolojia ya utangazaji wa redio kwa analojia itaendelea sambamba na redio kidijitali hadi hali ya soko itakavyoamua mwelekeo, inasisitiza ITU.[1]

Teknolojia ya redio kidijitali inaitwa DSB, kutokana na kifupisho chake kwa lugha ya Kiingereza, Digital Sound Broadcasting.

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya habari inakamilisha mipango ya ujio wa DSB nchini. Naibu Waziri, Mhe. Mhandisi Mathew Kundo alisema kwenye mkutano wa mwaka wa utangazaji uliofanyika Dodoma Februari 2024. [2].

Mhe. Kundo alieleza kuwa uamuzi wa kuikaribisha teknolojia ya utangazaji wa redio kidijiti unalenga kuleta utatuzi wa changamoto za sekta zikiwemo uhaba wa masafa ya utangazaji wa redio kwenye maeneo ya miji mikubwa ambayo hivi sasa inakabiliwa na uhaba wa rasilimali masafa. Aidha ujio wa teknolojia hiyo utawezesha ufikishaji wa matangazo ya redio kwa hadhira pana zaidi. Hii inatokana na teknolojia ya utangazaji wa kidijiti kutokuzuiwa na mipaka ya teknolojia, tofauti na utangazaji wa redio wa sasa unaotegemea rasilimali masafa ili kufikisha mawasiliano kwa wananchi.

Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza Mashariki na Kusini mwa Afrika kuhama kutoka utangazaji wa televisheni kwa mitambo ya ardhini wa analojia kwenda dijitali, baada ya kuzima mitambo ya analojia Disemba 2014, kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa kimataifa ya Juni 2015.

> Televisheni na redio ni aina mbili za utangazaji. Redio inafikia watu wengi zaidi na hivyo imeenea, na kufika, sehemu nyingi. Redio inaongoza kama chombo kikuu cha mawasiliano ya umma kutokana na kufika kwake kijiografia, vifaa vinavyotumiwa na wasikilizaji kubebeka kirahisi na kupatikana kwa bei nafuu zaidi ya televisheni.

Sambamba na huduma za utangazaji wa redio kupatikana kwenye vifaa vya kawaida na vilivyofungwa kwenye magari, redio pia zinasikilizwa kwenye simu za mkononi.

Utangazaji wa redio unatumia masafa ya mawasiliano kufikisha ujumbe. Kwa muda sasa, utangazaji wa redio umekuwa wa mfumo wa analojia. Aina ya mawimbi yanayotumika zaidi ni ya AM na FM.

Ingawaje mawimbi ya AM yanafika mbali zaidi, utangazaji wa FM unapendelewa zaidi kuliko AM kwani ina ustahimilifu zaidi na gharama za kuifunga ni chini kuliko AM. Vilevile radio za FM zinasikika sehemu nyingi zaidi na matangazo yake yana sauti bora zaidi.

Hata hivyo, nchi nyingi zimemaliza masafa ya FM yalizopangiwa na ITU.

Kuna uhaba wa yanayopatikana kwa watoa huduma wapya; hivyo kuwa na umuhimu wa kuanzisha teknolojia nyingine kuleta ufanisi kwenye utangazaji kwa redio.

**Megahezi (Mhz)**

**87.5-108**

Masafa ya FM yanayotumika Tanzania na Afrika yako kwenye bendi kuanzia megahezi (Mhz) 87.5 hadi 108.




Tekinolojia ya DSB inatumia masafa kwenye wigo wa kati ya megahezi **214** na **230**.

Kuna aina mbili za utangazaji wa redio kidijitali, yaani DSB. Hizo ni **DAB** na **DRM** ambazo ni vifupisho vya lugha ya Kiingereza vya Digital Audio Radio na Digital Radio Mondiale. Nchi nyingi za Afrika zinatumia DAB. Hata hivyo DSB inawakilisha utangazaji redio kidijitali. [3]

Mikakati ya Afrika kuanzisha na kuendeleza DSB imeandaliwa na Shirika la Afrika la Mawasiliano (ATU). Mpango mkakati wake unalenga kuhimiza nchi wanachama waanzishe utangazaji wa DSB ili angalau ifikapo 2024 angalau asilimia 56 ziwe na mipango ya kuanzisha teknolojia hiyo.

Misingi muhimu ya mkakati wa ATU ni pamoja na kuhimiza nchi za Afrika kutumia aina moja ya bendi za DSB na teknolojia zinazoambatana na matumizi ya bendi hizo. [4]

Nchi nyingi za Afrika zimeainisha mipango ya kuanzisha utangazaji wa DSB. Taasisi za ushirikiano kikanda zimelinganisha njia wanazotumia kufanikisha matumizi ya teknolojia hiyo.

Mifano ni Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kupitia Umoja wa Mawasiliano Afrika Mashariki (EACO) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kupitia CRASA – Chama cha wasimamizi wa sekta ya mawasiliano kwenye ukanda huo. Nchi wanachama zimeandaa mifumo ya utekelezaji itakayofanikisha kuanzisha huduma za DSB. [5]

Mawaziri wa mawasiliano wa SADC walipitisha azimio mwaka 2017 kuhusu DSB kama sehemu ya kuongeza ufanisi wa tekinoloja za utangazaji wa redio zilizoko nchini mwao.

Mawaziri walitambua kwamba ukanda wa SADC unasukumwa na umuhimu wa kuwa na huduma za utangazaji zinazotumia masafa kwa ufanisi. Vilevile waliona haja ya watoa huduma za utangazaji kupanua wigo wa utoaji huduma ili kukidhi mahitaji ya umma, na ya jamii kuweza kutuma na kupokea taarifa wakati wa dharura na maafa.

Hatua yao ilifuatia utambuzi kuwa mahitaji ya huduma za utangazaji wa redio yanayozidi kukua yamezidi upatikanaji wa masafa ya FM.

Madhumuni mengine yalikuwa ni kuhakikisha ufanisi kwenye matumizi ya masafa adimu ya utangazaji na kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya huduma za utangazaji kwa redio.

Akizungumzia ufanisi wa matumizi ya masafa kwenye utangazaji redio kidijitali, Meneja wa Kitengo cha TCRA cha Huduma za Utangazaji, Mhandisi Andrew Kisaka alieleza kuwa safa moja chini ya teknolojia hiyo litaweza kuzalisha vituo 14 vya utangazaji, hivyo kuwezesha ongezeko la idadi ya vituo vya utangazaji.

Tunatarajia kwamba rasilimali moja ya masafa itawezesha vituo angalau 14 kutoa huduma, na hii itaondoa kikwazo cha ukosefu wa masafa hasa kwenye maeneo ya miji kama vile Dar es salaam, Mwanza, Dodoma na miji mingine," alieleza.

Baadhi ya nchi za SADC na EAC zimeanza ama kutangaza kwa majaribio katika miji mikubwa kutumia DSB au kuanzisha majadiliano ya wadau kuhusu rasimu za kanuni na utaratibu wa kutoa leseni kwa huduma za utangazaji kwa redio kidijitali.[6]

Majaribio yanayofanyika yanapima sifa za teknolojia hiyo na kuangalia utayari wa wasikilizaji na wadau wengine na kupata mrejesho kutoka kwao. Utangazaji huo wa majaribio pia unawezesha nchi hizo kuendeleza uandaaji wa maudhui yanayotolewa kidijitali na kuelewa gharama za kuanzisha teknolojia hiyo.

Vile vile majaribio yatawezesha kuelewa masuala ya mapato ya watoa huduma, kuweka misingi ya sera na mahitaji ya kiusimamizi kabla ya kuanzisha huduma za utangazaji wa DSB kwenye nchi husika.

Mamlaka ya Mawasiliano Kenya (CA) imeweka mfumo wa utekelezaji wa uanzishaji huduma za utangazaji wa DSB nchini humo ifikapo mwaka 2025.

Mfumo huo unachambua njia mbalimbali na mahitaji ya kuanzisha DSB kama njia ya ziada ili kubadili utangazaji wa redio Kenya, Mkurugenzi Mkuu wa CA ameeleza.

Kenya imetambua changamoto zitakazojitokeza wakati wa kutekeleza DSB kwa teknolojia ya DAB. Hizo ni pamoja na uwezekano wa baadhi ya wadau kupinga mfumo wa utaratibu mpya wa uendeshaji shughuli za redio kidijitali, na masuala ya upatikanaji na unafuu wa redio zinazowezesha kupatikana matangazo hayo.

Changamoto nyingine ni gharama za miundombinu mipya, uwezo wa kifedha kueneza huduma na umuhimu wa kushawishi watoa huduma kutumia teknolojia mpya hasa kwa kuwa hakuna tarehe au mpango wa kuzima matangazo ya FM. [7]

Tume ya Utangazaji Uganda imeanzisha matangazo ya majaribio kwa teknolojia ya DAB kwenye eneo la kilometa za mraba 80 kuzunguka jiji la Kampala. Uwezo na ufanisi wa teknolojia hiyo vitapimwa. [8]

Afrika Kusini, kupitia msimamizi wa mawasiliano – ICASA- imetoa mwongozo na kanuni za kuanzisha huduma za utangazaji wa redio kidijitali. Kanuni zinaainisha utaratibu wa kuomba leseni na kutoa huduma za DSB. [9]

Ghana imekuwa nchi ya kwanza Afrika Magharibi kujaribu matangazo ya DSB kupitia vituo 18 vilivyopo, 11 vikiwa jijini Accra, mji mkuu wa nchi hiyo. Redio hizo zilitumia transmita moja na chaneli moja ya masafa kwenye bendi ya Mrudio wa Juu Sana (VHF) kwenye megahezi **174** hadi **230**. [10]

Ufanisi kwenye kuanzisha na kuendelea utangazaji wa redio kidijitali utahitaji nchi husika kujipanga upya kisheria na kiusimamizi. Itabidi kupitia upya mifumo ya uendeshaji wa huduma za utoaji maudhui ya utangazaji wa redio.

Hii ni pamoja na kupanga upya matumizi ya masafa, kuweka kanuni na kushirikisha wadau katika mnyororo wote wa utangazaji wa redio.

## Rejea


(tovuti zote zilitembelewa Februari 2024)

1. https://www.itu.int/en/ITU-D/Technology/Pages/Broadcasting.aspx
2. https://www.tcra.go.tz/tcra-news/tanzania-tunes-in-to-the-future-with-digital-sound-broadcasting-dsb.
3. https://www.rfwireless-world.com/Terminology/Advantages-and-disadvantages-of-DAB.html
4. https://atuuat.africa/wp-content/uploads/2023/05/ATU-R-Strategy-002-0-Strategy-on-Introduction-and-Promotion-of-DSB-in-Africa.docx.pdf
5. https://eaco.int/admin/docs/publications/Harmonised%20Framewrk%20for%20Digital%20Sound%20Broadcasting.pdf.
6. https://www.crasa.org/post-articles/framework-on-establishment-of-digital-sound-broadcasting-in-sadc-edition-2017
7. https://repository.ca.go.ke/handle/123456789/101
8. https://www.ucc.co.ug/broadcasting/DAB Pilot Project
9. https://www.gov.za/sites/default/files/gcis_document/202104/44469gen215.pdfhttps://www.sadiba.org/images/PDFfiles/Gov_Policy_on_Digital_Radio_10_March_2020.pdf
10. https://nca.org.gh/2023/08/22/trial-phase-of-digital-audio-broadcasting-dad-launched-in-ghana/

UTANGAZAJI

# Faida utangazaji wa redio kidijitali

Na Mwandishi wetu

Utangazaji wa redio kidijitali (DSB) utaleta faida kwa watoa huduma za utangazaji, wasikilizaji, msimamizi wa sekta, Serikali, waagizaji wa vifaa vya utangazaji na wahusika wengine kwenye mnyororo wa utangazaji. Hawa ni pamoja na watengenezaji maudhui, waendeshaji mitambo ya kurushia matangazo na waagizaji na wazuaji wa vifaa vya utangazaji.

## Watoa huduma za utangazaji

1. Huduma za redio kidijitali zinazotumia teknolojia ya DAB zinatumia masafa kwa ufanisi. Mifumo yake inaweza kutoa huduma za utangazaji wa vituo vingi vya redio kwa mara moja kutumia safa moja.
2. Mfumo wa DSB una gharama za uendeshaji kidogo zaidi ya FM na hazitegemei mtaji mkubwa.
3. Vituo vya DSB vina gharama kidogo za kusambaza maudhui na vinatumia nishati kwa ufanisi zaidi.
4. Mfumo wa DSB unatoa fursa mpya za uvumbuzi na ubunifu. Watoa huduma wanaweza kuwa na redio nyingi za kidijitali badala ya kituo kimoja cha redio cha analojia.
5. DSB inachagiza uwekezaji kwenye huduma za maudhui kwa kuwa zinahimiza uchangiaji wa miundombinu kupitia wasambazaji wa maudhui.

## Watumiaji/ wasikilizaji

1. Redio chini na mfumo wa DAB zinawezesha sauti bora zaidi kuliko inayotoka kwenye matangazo ya AM na FM
2. Hakuna muingiliano wa sauti, mikwaruzo au kelele.
3. Huduma zinaaminika zaidi na ni rahisi kutumia.
4. Stesheni za DAB ni rahisi kutafuta na zinapatikana kwa urahisi. Aidha zinaweza kupangwa kuanza zenyewe kutoa maudhui kadri mtumiaji anavyopenda.
5. Vituo vya DAB vinawezesha msikilizaji kuwa na chaguo pana la vituo tofauti vya kusikiliza.
6. Mfumo wa DAB unawezesha matumizi ya vifaa
7. vingi kupokelea matangazo. Hivi ni pamoja na visivyobebeka, vinavyobebeka na vya mkononi.

## Mchango kwa uchumi

1. Mfumo wa utangazaji wa DSB unatoa fursa za kuzalisha ajira za kutengeneza na kusambaza maudhui.
2. Kuna fursa nyingi kwenye mnyororo wa utoaji huduma za redio kidijitali. Mifano ni kuagiza na kusambaza vifaa vya utangazaji na vya kupata maudhui.
3. Kutokana na ufanisi kwenye matumizi ya nishati, mfumo wa DSB unawezesha nishati ya ziada kupatikana na kuelekezwa kwenye shughuli nyingine za kiuchumi.

## Matatizo/changamoto/vikwazo

Pamoja na faida zake, mfumo wa utangazaji wa DSB unaweza kuwa na matatizo kwenye nchi husika miaka ya mwanzoni. Haya ni pamoja na uwezekano wa kutokuenea sehemu nyingi, kutokupatikana kwa matumizi na mitambo na vifaa kutokuingiliana.

Wasikilizaji wenye vifaa vya mkononi wanaweza wasipate matangazo bila kukatika mara kwa mara. Aidha kwenye nchi zilizoanza huduma ya DAB kumekuwa na malalamiko ya sauti kutokuwa nzuri ikilinganishwa na matangazo ya FM.

Vilevile kumekuwa na malalamiko ya muingiliano wa sauti, na kelele. Watumiaji wengine wametaja tatizo la betri za vifaa vya DSB kumalizika chaji haraka kuliko za vifaa vya utangazaji wa AM au FM.

Pamoja na yote hayo, mifumo ya utekelezaji wa mipango ya kuanzisha huduma za DSB kwenye nchi husika inatakiwa kuweka sawa masuala ya kiufundi, kisheria na kiusimamizi. Viwango vya ubora wa vifaa na huduma vinatakiwa kuwekwa.

# Maadili ajenda kuu mkutano wa utangazaji 2024

Na Mwandishi wetu

Umuhimu wa kuthibiti mmomonyoko wa maadili ya utangazaji umejitokeza kwenye mada na majadiliano katika mkutano wa mwaka wa wataalamu wa masuala ya habari na usimamizi wa taasisi zinazojihusisha na sanaa na maudhui Tanzania.

Mada karibu zote zilizowasilishwa kwenye mkutano huo wa mwaka Dodoma Februari 2024 ziligusia maadili na umuhimu wa kuendeleza utamaduni na tunu za Kitanzania.

Akiwasilisha mtazamo wa mdhibiti wa sekta, Mkurugenzi wa huduma za kisheria kutoka TCRA, Dkt Philip Filikunjombe alitaja mambo matano yanayoathiri ubora wa utangazaji na kutokea hali ya kutokuzingatia maadili.

Alieleza kuwa jamii imeendelea kushuhudia kukua na kuongezeka kwa hali ambayo kila mtu anaweza X Alieleza kuwa uandishi mitandaoni umejikita zaidi kwenye 'ukimbizaji' wa matukio badala ya kujadili matukio, maudhui yenye mashaka na yasiyokuwa na tija, kutokuzingatia haki ya kujibu tuhuma na uwekaji na urushaji maudhui muda usiofaa.

Aliongeza kwamba kumekuwa na mahaba na chanzo kimoja cha habari na "kuruhusu chanzo kimoja kuzungumza mwanzo hadi mwisho".

Kutozingatiwa kanuni za utangazaji kumeongezeka, alisema na kutoa mfano wa kuibuka aina mpya ya utangazaji usiozingatia misingi ya maadili ya taaluma hiyo.

Akiwasilisha mada kuhusu maadili ya utangazaji kwenye vyombo vya habari vya mtandaoni, mtaalamu wa mawasiliano na mwalimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dkt Abdallah Katunzi alifafanua kwamba pamoja na mabadiliko ya teknolojia yaliyowezesha kuwepo vyombo vya mtandaoni, misingi ya taaluma na maadili ya uandishi na utangazaji havijabadilika.

Alieleza kuwa uandishi mitandaoni umejikita zaidi kwenye 'ukimbizaji' wa matukio badala ya kujadili matukio, maudhui yenye mashaka na yasiyokuwa na tija, kutokuzingatia haki ya kujibu tuhuma na uwekaji na urushaji maudhui muda usiofaa.

Aliongeza kwamba kumekuwa na mahaba na chanzo kimoja cha habari na "kuruhusu chanzo kimoja kuzungumza mwanzo hadi mwisho".

> Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Dkt Kedmon Mapana alibainisha maadili kuwa ni tabia njema, misingi na mienendo inayokubalika kulingana na mila na desturi za jamii husika. Vilevile ni msukumo wa kutenda jambo sahihi, mahali sahihi na wakati sahihi.

Uzingatiaji wa maadili ni muhimu ili kulinda jamii, hasa watoto na vijana, alieleza.

Alitaja vigezo 12 vya maadili kwenye sanaa na masuala yanayosimamiwa na BASATA. Kwa kiasi kikubwa vinafanana na vingi kwenye Kanuni zinazosimamiwa na TCRA.

1. Sanaa inatakiwa izingatie masharti ya sheria za nchi;
2. Isishawishi vitendo vya kihalifu;
3. Isichochee ghasia;
4. Isihamasishe ngono, ushoga, usagaji, na madawa ya kulevya;
5. Isivunje utu na heshima ya mtu;
6. Isiwe ya uchochezi au upotoshaji;
7. Isiwe na maneno ya uongo, uchochezi au kashfa kwa watu;
8. Isiwe na ujumbe wa unyanyasaji na ukatili;
9. Isitumie lugha chafu au matusi;
10. Isitukuze ubaguzi, udini na ukabila;
11. Isikashifu Taifa la Tanzania au mataifa mengine na
12. Isidhoofishe umoja, ushirikiano na ustawi wa jamii.

Tanzania itafanya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani. TCRA inasimamia Kanuni za huduma za utangazaji maudhui na utangazaji

wa uchaguzi wa vyama vya siasa.

Akiwapitisha washiriki kwenye kanuni hizo, Meneja wa TCRA wa Huduma za Utangazaji, Mhandisi Andrew Kisaka alisema vyombo vya utangazaji vina majukumu ya kutoa elimu kwa wapiga kura, kufahamisha umma mwenendo wa kampeni za vyama, na kuripoti hali halisi siku ya kupiga kura na matokeo yanapotangazwa.

Kanuni zinalenga kuviwezesha vyombo vya utangazaji kuweka mizania ya matangazo, na kutokubagua kundi lolote katika jamii wakati wa uchaguzi ili kuhakikisha haviegemei upande wowote.


Pia zinataka vyombo vya utangazaji kuhamasisha weledi na maadili ya utangazaji.

Changamoto ya fedha kwa shughuli mbalimbali kwenye mnyororo wa utoaji maudhui zilijadiliwa na Afisa Mikopo wa Mfuko wa Maendeleo ya Utamaduni na Sanaa, Bi Flora Kawiche.

Alisema Mfuko huo unatoa mikopo ya kati ya shilingi **200,000** hadi **100,000,000** hadi miaka miwili, kwa riba ya asilimia tisa **(9%)** kwa mwaka. Walengwa wa mikopo hiyo ni vyombo vya utangazaji na watengenezaji maudhui.

Lengo ni kuhakikisha taswira ya Tanzania kama jamii inawakilishwa ipasavyo katika vyombo vya habari na kwenye maudhui yanayotengenezwa na kusambazwa, alieleza.

Mfuko umewezesha miradi 173 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.8, aliongeza.




Akizungumzia Maudhui bora ya ndani na uchumi wa kidijitali, Bi Lilian Urio, mtaalamu na mtayarishaji maudhui, alisema maudhui bora ya ndani ni muhimu kwa kuwa yachangia kukua kwa uchumi wa Tanzania. Aliongeza kuwa yanaimarisha ustawi wa taifa na usalama wa watu wake.

## Tanzania mjumbe vyombo vya mikakati TEHAMA kimataifa



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) Dkt Jabiri Bakari ameteuliwa mjumbe wa bodi ya chombo cha Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) kinachoshughulikia maendeleo ya uvumbuzi na ubunifu katika teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Jina kamili la chombo hicho cha ITU ni Bodi ya Uvumbuzi wa Kidijiti ya Muungano wa Uvumbuzi na Ujasiriamali kwa Maendeleo ya Kidijiti.

Bodi hiyo ilifanya mkutano wake wa kwanza makao makuu ya ITU, Geneva, Uswisi Machi 2024 ambako washiriki walisisitiza umuhimu wa vipaumbele kwenye uvumbuzi wa kidijitali unaolenga kutatua changamoto za jamii, na haki za wavumbuzi.

Pamoja na Dkt Bakari, washiriki wengine kutoka Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya TEHAMA Dkt. Nkundwe Mwasaga, na Mkurugenzi wa TCRA wa Masuala ya Kisekta, Mhandisi Mwesigwa waliwakilisha Tanzania.

Tanzania ni mjumbe wa vyombo mbalimbali vya taasisi za kimataifa vya TEHAMA na masuala ya Posta. Taasisi hizo ni pamoja na ITU, Umoja wa Mawasiliano ya Simu Afrika (ATU),Umoja wa Posta Ulimwenguniu (UPU) na Umoja wa Posta Afrika (PAPU).

Ushiriki huo ni sehemu ya mikakati ya serikali ya Awamu ya Sita kuinua hadhi ya Tanzaniua kimataifa.

# Wito Bodi ya Ithibati iharakishwe

Na Mwandishi wetu

Washiriki wa mkutano wa mwaka wa utangazaji, ulioandaliwa jijini Dodoma Februari 2024 na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ulipitisha maazimio 17 kuhusu weledi, maudhui, kanuni, masuala ya uendeshaji na usimamizi wa sekta.

1. Vyombo vya Habari viajiri waandishi wa Habari wenye vigezo, maadili na taaluma ya uandishi wa habari.
2. Bodi ya ithibati iundwe na vyama vya kitaaluma vitumike kutoa maoni kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Bodi hiyo.
3. Vyombo vya Utangazaji viwe na mwongozo wa uendeshaji unaozingatia maadili.
4. Mamlaka iangalie ukomo wa leseni za utangazaji wa maudhui ya televisheni na Redio ambao kwa sasa ni miaka mitano.
5. TCRA kufuatilia kuhusu tozo na kodi za visimbuzi zinazohusiana na "eco levy".
6. TCRA kupitia na kuharakisha mapendekezo na marejeo ya Kanuni kuhusu leseni za utangazaji kwa njia ya televisheni (kutoka FTA kwenda Free to View).
7. TCRA kuongeza ushirikishaji wa wadau wakati wa kufanya marekebisho ya mifumo ya leseni za Utangazaji.
8. TCRA kuangalia uwezekano wa kuchangia gharama za ushiriki wa vituo vya Utangazaji kwenye mkutano wa mwaka wa utangazaji (ABC) ili vituo vingi viweze kuhudhuria.
9. Maazimio ya mwaka 2023 ambayo hayajafanyiwa kazi ipasavyo yaendelee kufanyiwa kazi na vyombo vya habari.
10. Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari iangalie uwezekano wa kuelimisha taasisi za serikali kuhusu kutoa ushirikiano kwa waandishi wa Habari wanapotaka ufafanuzi wa mambo yanayozihusu taasisi husika.
11. Vyombo vya Habari kuwa na sera za uhariri za vituo inayotekelezeka na kutoa mafunzo ya ndani kwa wafanyakazi wake kuhusu sera na miongozo ya chombo husika.
12. Vyombo vya Habari vihakikishe vinazingatia hatua zote muhimu za kutafuta, kuchakata na kuwasilisha maudhui.



*Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa ndani ya studio za redio ya jamii, Ruangwa, Lindi.Alifuatana na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M Nnauye ( wa pili kulia waliosimama).*

13. TCRA iweke msisitizo maalumu katika kufuatilia na kuvisimamia vyombo vya Habari vya mtandaoni ili viweze kufuata maadili na taaluma ya utangazaji.

14. Vyombo vya Habari kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake ili kuviwezesha kufanya kazi zake kwa weledi.

15. TCRA kufanya tafiti kuangalia viwango vya ubora vya vituo vya utangazaji pamoja na utafiti wa hadhira.

16. TCRA kupeleka ombi kwenye mamlaka husika kuhusu punguzo la ushuru za umeme kwa ajili ya kuendesha mitambo ya utangazaji.

17. Vyombo vya utangazaji kutumia uzoefu na ushauri uliotolewa na wakongwe kwenye sekta ya utangazaji ili kutambua mchango wao kwenye sekta ya utangazaji.

## Rejea/Ufafanuzi

1. Sheria ya Huduma za Vyombo vya habari ya 2016 inataka kuwe na Bodi ya Ithibati ambayo ina majukumu ya:

- Kusimamia kanuni za maadili ya wanahabari.
- Kutoa ithibati na vitambulisho kwa wanahabari.
- Kusimamia viwango na mienendo ya kitaaluma na kuendeleza vigezo bora vya maadili na nidhamu miongoni mwa wanahabari.
- Kushauri serikali katika mambo yanayohusiana na elimu na mafunzo ya wanahabari.
- Kushauri serikali katika mambo yanayohusiana na elimu na mafunzo ya wanahabari.
- Kutunza orodha ya wanahabari waliothibitishwa.

Katika kutekeleza kazi zake, Bodi itakuwa na Mamlaka ya kuwasimamisha au kuwaondoa wanahabari walio thibitishwa katika orodha na pia kutoa adhabu kwa wanaokiuka kanuni.

2. Hii ni tozo ya mazingira ambayo inatozwa kwa vifaa vya kielektroniki vinavyoingia Tanzania kuwezesha kifedha mfumo wa kuchakata na kuvitupa vitakapokuwa taka za kielektroniki.

Wanaolipia tozo hiyo ni watengenezaji na wauzaji wa vifaa hivyo.

Hizi ni taka zinazotokana na vifaa au vijenzi vya vifaa vya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) vikiwemo simu za mkononi, kompyuta, vifaa vya mawasiliano ya simu, televisheni na redio.

Hoja ilitolewa na wasambazaji wa maudhui ambao walilalamika kwamba tozo ya ving'amuzi ni kubwa ukilinganisha na simu za mkononi hata zinazouzwa ghali zaidi ya ving'amuzi.



*Baadhi ya wanahabari wastaafu wa iliyokuwa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) wakiwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasilisno Tanzania (TCRA) Dkt Jabiri Bakari walipomtembelea hivi karibuni. Wanataaluma hao wameanzisha Chama cha Wakongwe wa RTD kwa lengo la kuhimiza weledi kwenye utangazaji.*

# Kanuni kuongeza ufanisi matumizi postikodi

**Sehemu hii ya jarida ni mahsusi kuelezea mabadiliko ya hivi karibuni kwenye sheria na masuala ya usimamizi Tanzania. Makala hii inaangalia marekebisho ya Kanuni zinazohusu Posta.**

TCRA ina jukumu, chini ya Sheria ya Mawasiliano na Kielektroniki na Posta (sura ya 306 ya sheria za Tanzania) kutenga, kugawa, kusimamia na kuthibiti anwani na postikodi. Vilevile imepewa uwezo wa kusimamia uchapishaji na uuzaji wa orodha za postikodi na vitabu vya anwani kwa kuzingatia misingi ya usambazaji.

Watoa huduma za posta wanatakiwa kuweka vitabu vya anwani za kufikisha vitu kule vinapotumwa, na postikodi, na kuwezesha hivi kupatikana kwa jamii bila malipo.

Kanuni za Mawasiliano ya Kieketroniki na Posta kuhusiana na masuala ya Posta zimerekebishwa ili kuboresha matumizi ya mifumo ya anwani na kuanzisha utaratibu wa kutumia postikodi kibiashara.

Januari 2024, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape M. Nnauye alichapisha Notisi namba 18 ya 2024 kwenye Gazeti la Serikali kuhusu marekebisho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kieketroniki na Posta kuhusiana na masuala ya Posta.

Kanuni ya 28 ya toleo la 2018 la Kanuni tajwa imerekebishwa kwa kuongeza sehemu inayoainisha yafuatayo:

TCRA inaweza kutenga na kugawa postikodi katika makundi matano kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Postikodi zitakuwa za:

a. Maeneo ya Kiutawala, ambazo zitatolewa kwa Kata.
b. Ofisi za Posta, ambazo zitatolewa kwa ofisi za Posta.
c. Taasisi zinazotuma na kupokea vitu vingi kwa posta, ambazo zitatolewa kwa baadhi ya ofisi za taasisi za Serikali.
d. Maeneo maarufu, ambazo zitatolewa kwa maeneo maalum.
e. Shughuli au matukio maalum, ambazo zitatolewa kwa muda kwa matukio maalum. Hizi zitalipiwa ada zilizoainishwa kwenye nyongeza ya Kanuni zilizorekebishwa.

TCRA inagawa na kutoa postikodi bila malipo kwa maeneo ya Kiutawala, ofisi za Posta, taasisi zinazotuma na kupokea vitu vingi kwa posta, na maeneo maarufu kutegemea maeneo yao ya makazi au shughuli na aina zake.

## Postkodi kwa shughuli au matukio 'maalum'

TCRA sasa inagawa na kutoa postikodi kwa ajili ya shughuli au tukio maalum kwa mtu binafsi au kampuni inayoendesha shughuli au tukio husika kibiashara. Mhusika atalipa ada zilizoainishwa kwenye nyongeza ya Pili ya Kanuni tajwa.

Waombaji wanatakiwa kutaja kwa usahihi na kueleza shughuli inayoombewa postikodi, ikiwa na pamoja na muda wote wa shughuli au tukio na nyaraka za idhini kutoka kwa Serikali za Mtaa eneo husika.

Vilevile, waombaji wanatakiwa kueleza mahali shughuli au tukio lilipo kijiografia (kwa kutaja latitudo na longitudo). Muda wa juu wa vibali vya matumizi ya postikodi za shughuli ni siku 30, lakini zinaweza kuongezwa kwa maombi iwapo shughuli itapitiliza muda huo.

TCRA inawakaribisha watu binafsi na kampuni zinazokusudia kutangaza matukio yao au shughuli kuomba postikodi za matukio. Haya ni ni pamoja na burudani, maonesho, tamasha shughuli za kidini.

Postikodi inawezesha wateja na walengwa wa shughuli husika kufika kwenye eneo lililopangwa kwa urahisi, na pia zinaharakisha uchambuaji na ufikishaji wa nyaraka na vitu vinavyotumwa kuhusiana na shughuli hizo.

# Azma ya mabadiliko kidijitali

Na Mwandishi wetu

**Takwimu zinazowasilishwa humu zinaonesha mwelekeo wa ukuaji wa sekta ya mawasiliano ndani ya miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan (Machi 2021 hadi Machi 2024)**

Kuenea simu zenye uwezo mkubwa, maarufu kama simu janja miongoni mwa watu kumeongezeka kutoka asilimia 15 hadi 32 kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023 na kuzidi kuongeza kasi ya matumizi ya intaneti kupitia vifaa vya mkononi.

**99.8%**

Asilimia 99.8 ya watumiaji wa intaneti wanapata huduma hiyo kupitia vifaa vya mkononi, zikiwemo simu na vishikwambi.

Laini za simu 35,885,592 zilitumika kupata huduma ya intaneti Desemba 2023 ikilinganishwa na 29,103,482 Desemba 2021. Desemba 2022 zilikuwa 31,172,544.

**Laini za simu zilizopata huduma ya intaneti**



| | |
|---|---|
| **Desemba 2023** | **35.8 milioni** |
| **Desemba 2022** | **31.1 milioni** |
| **Desemba 2021** | **29.1 milioni** |

Takwimu za mawasiliano za Desemba 2023 zilizotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaonesha kuwa watumiaji wa intaneti Tanzania wanatumia asilimia 24 tu ya uwezo uliopo wa intaneti ya kimataifa. Kuna ongezeko kidogo kutoka asilimia 23 ya mwaka 2022. Matumizi haya yanapimwa kwa kipimo cha Gbps.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dkt. Jabiri Kuwe Bakari amesema kwenye taarifa ya Mamlaka ya robo mwaka ya Oktoba hadi Desemba 2023 kwamba taasisi yake itafuatilia kwa kina gharama za simu janja kwani kutokuenea kwa simu janja kwa watumiaji wengi ni mojawapo ya sababu za kutokuenea kwa matumizi ya intaneti kwa kasi.

> Uwiano kati ya mitandao na matumizi ya intaneti unaonesha kuwa maeneo mengi yamefikiwa na huduma za intaneti ila kuna watumiaji wachache; sababu ikiendelea kuwa ni idadi ndogo ya watumiaji wenye simu janja.
>
> — Dr Jabiri Kuwe Bakari
>
> *TCRA Director General*

Upatikanaji wa masafa zaidi yanayowezesha intaneti ya kasi (5G) utachochea kukua kwa matumizi ya intaneti. Tanzania imepata masafa mapya yatakayowezesha huduma ya uzao huo, ambayo ni muhimu katika kuchochea uchumi wa kidijitali.

Masafa hayo yalitolewa kwenye mkutano wa kila miaka minne wa masuala ya masafa unaoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mawasiliano (ITU) uliofanyika Dubai Falme za Kiarabu Desemba mwaka jana.


Vidokezi vya ukuaji wa sekta vinaonesha mabadiliko ya kasi kwenye maeneo mengi. Kwa mfano, huduma za utangazaji wa televisheni zimezidi kuimarika kutokana na kuongezeka matumizi ya ving'amuzi. Sekta ndogo ya posta imeonesha mwanga wa mabadiliko.

Takwimu za TCRA za Oktoba hadi Desemba 2023, zinaonesha kasi ya usajili wa akaunti za pesa kwa simu za mkononi ilizidi ile ya usajili wa laini za simu kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023. Hii inaashiria kwamba watumiaji wengi wa simu za mkononi wanajisajili kwa huduma za fedha mtandaoni na kidijitali.

Wakati usajili wa laini za simu uliongezeka kwa wastani wa asilimia 11.17 kati ya Desemba 2021 na Desemba

2023, usajili wa akaunti za fedha kidijitali uliongezeka kwa wastani wa asilimia 18.17. Watumiaji wa huduma za fedha wanatakiwa kujisajili.

Laini za simu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka 54,044,384 ambazo zilienea kwa asilimia 91 miongoni mwa Watanzania Desemba 2021 hadi 70,292,899 zilizoenea kwa asilimia 111 Disemba 2023, takwimu hizo zinaonesha.



Vilevile taarifa hiyo inaonesha kwamba akaunti za pesa kwa simu na idadi ya miamala viliongezeka zaidi ya mara mbili kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023.

Akaunti zimeongezeka kutoka 35,285,767 zilizofanya miamala 3,752,084,894 hadi 52,875,129 zilizofanya miamala 5,273,086,154 kipindi hicho.

Huduma za fedha mtandao zimezalisha ajira nyingi, zikiwemo za wakala. Vilevile benki nyingi zimeboresha na kurahisisha huduma zake ambapo zinawatumia watoa huduma hawa kama wakala wao ili kufikisha huduma za kibenki karibu na wateja wao.

Pamoja na kuleta ufanisi, huduma za fedha kupitia simu za mkononi pia zimepunguza kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji kwa taasisi, hasa baada ya serikali kuanzisha mfumo wa malipo ya kiserikali mtandaoni (GePG).

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za simu za mkononi na kuwapa namba za mawasiliano na misimbo, au namba fupi ya kuwezesha miamala hiyo.

Benki Kuu ya Tanzania inasimamia sekta ya fedha kwa ujumla na inatoa leseni za huduma za fedha mitandaoni.

Taasisi hizi zinashirikiana kwenye masuala ya fedha mtandaoni.

Pamoja na kukua kwa huduma za pesa mtandao, gharama za mawasiliano zimeshuka ndani ya miaka mitatu iliyopita. Hizi ni pamoja na gharama za kupiga simu nchi za Afrika Mashariki.

Takwimu za Desemba 2023 zinaonesha kuwa dakika za simu za kimataifa zinazoingia nchini zimeongezeka kwa asilimia 29.2; kwa kipindi kifupi; kutoka 2,216,904 Septemba 2023 hadi 3,129,711 Desemba 2023.

## Jedwali 1: Uwezo/upatikanaji wa intaneti ya kimataifa na matumizi hadi kufikia Desemba 2023. Kipimo cha Gbps

| | Uwezo wa intaneti zinazotoka | Uwezo wa kuingiza intaneti |
|---|---|---|
| | 2023 | 2023 |
| Jumla | 4,750 | 4,750 |
| Inayotumika | 771 | 771 |
| Inayopatikana kwa watumiaji wapya | 3,979 | 3,979 |

Chanzo: TCRA

**Jedwali 2: Kuenea kwa teknolojia ya mawasiliano Desemba 2020, Desemba 2021, Desemba 2022 na Desemba 2023**

| Na | Maelezo | Mwaka/Asilimia (%) | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Desemba 2020 | Desemba 2021 | Desemba 2022 | Desemba 2023 |
| 1 | Kuenea uzao wa pili (2G) miongoni mwa watu | 94% | 95% | 95% | 98% |
| 2 | Kuenea uzao wa tatu (3G) miongoni mwa watu | 59% | 63% | 72% | 86% |
| 3 | Kuenea uzao wa nne (4G) miongoni mwa watu | 33% | 47% | 55% | 79% |
| 4 | Kuenea Kijiografia | 63% | 65% | 66% | 73% |
| 5 | Kuenea Simu zenye uwezo mkubwa(simu-janja) | - | - | 25% | 32.12% |

Dkt Jabiri amefafanua kuwa kuongezeka kunasababishwa na mabadiliko yanayoendelea ya kuoanisha upigaji simu ndani ya nchi za Afrika Mashariki, ambapo kwa sasa mtumiaji anapiga simu kwenda nchi nyingine ukanda huu kama yuko nchini kwake.

Juhudi za kukabiliana na simu za ulaghai na zinazotumika kwa utapeli zinaelekea kuzaa matunda kutokana na kupungua kwa matukio yaliyoripotiwa.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, simu za ulaghai zimeshuka kutoka asilimia 2 ya idadi ya laini za simu zilizosajiliwa Septemba 2022 hadi asilimia 0.01 Desemba 2023. Simu za ulaghai zilianza kupungua Novemba 2022.

Simu zilizofungiwa baada ya kuripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu pia zilipungua kwa asilimia 13.03 kati ya Septemba na Desemba 2023.

Namba tambulishi zilizofungiwa kati ya Oktoba na Desemba 2023 baada ya kuripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu zimepungua kwa asilimia 13. Laini 30,309 zilifungiwa Desemba ukilinganisha na 34,848 zilizofungiwa Septemba 2023. Laini zinafungiwa kuwezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko.

Wakati huo huo leseni za huduma kuu za mawasiliano ya simu, intaneti, maudhui ya utangazaji na posta na usafirishaji wa vifurushi zimeongezekau; hasa zile za programu tumizi za mawasiliano, ambazo zoinawezesha matumizi ya intaneti.


Kwa uwiano, TCRA imetoa leseni nyingi za huduma tumizi za mawasiliano, ambazo zinachangia katika kuendeleza huduma za intaneti. Huduma zinazotolewa chini ya leseni za kutumia miundombinu kutoa huduma ni pamoja na simu za mkononi, ambazo idadi ya watoa huduma wake haijabadilika sana.

**Jedwali 3: Mwelekeo wa usajili wa laini, akaunti za pesa kwa simu, idadi ya miamala kati ya Desemba 2021 na Desemba 2023**

| Mwaka | Akaunti | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) | Laini za simu | Ongezeko | Asilimia ya ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Desemba 2021 | 35,285,767 | 3,017,137 | 9.35 | 54,044,384 | 2,824,151 | 5.51 |
| Desemba 2022 | 40,953,496 | 5,667,729 | 16.06 | 60,192,331 | 6,147,947 | 11.37 |
| Desemba2023 | 52,875,129 | 11,921,633 | 29.11 | 70,215,144 | 10,023,034 | 16.65 |
| Wastani wa asilimia ya ongezeko | | | 18.17 | | | 11.17 |


# Takwimu za Mawasiliano katika namba

## Takwimu za usajili wa simu



Milioni **70.3**

Desemba 2023



**3.1%**


Milioni **72.5**

Machi 2024

## Usajili wa laini za simu kwa ajili ya P2P na M2M kwa kila mtoa huduma

| Mtoa huduma | Vodacom | Halotel | TTCL | Airtel | Tigo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| M2M | 522,381 | 55,350 | 6,544 | 320,471 | 24,937 | **929,683** |
| P2P | 22,106,960 | 9,298,742 | 1,669,997 | 19,144,882 | 20,275,514 | **72,496,095** |
| **Jumla** | **22,629,341** | **9,354,092** | **1,676,541** | **19,465,353** | **20,300,451** | **73,425,778** |

## Mgawanyo wa usajili wa laini kwa watoa huduma







Takwimu za P2P zinaonesha kuwa hakuna mtoa huduma aliyezidi **35%**, ambayo ni kiwango cha chini cha umiliki wa soko. Hii inaonesha kuna **ushindani wenye tija** kati ya watoa huduma

## Takwimu za Pesa Mtandao

**0.2%**




## Usajili wa vipokezi vya posta

### Masanduku na mifuko binafsi ya barua

| Mwezi | Masanduku ya barua | Mifuko binafsi ya barua |
|---|---|---|
| Januari | 158,183 | 10,000 |
| Februari | 158,183 | 10,000 |
| Machi | 316,182 | 10,069 |